

SURA YA 423

SHERIA YA KUZUIA UTAKATISHAJI WA FEDHA HARAMU

[SHERIA KUU]

MPANGILIO WA VIFUNGU

Kifungu                      Jina

SEHEMU YA I

VIFUNGU VYA AWALI

1. Jina fupi
2. Matumizi
3. Tafsiri

SEHEMU YA II

KITENGO CHA KUDHIBITI BIASHARA YA FEDHA HARAMU NA KAMATI YA TAIFA

4. Uanzishwaji wa Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu
5. Uteuzi wa Kamishina
6. Mamlaka na Majukumu ya Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu
7. Watumishi wa Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu
8. Uanzishwaji na Muundo wa Kamati ya Taifa
9. Kazi za Kamati ya Taifa
10. Vikao vya Kamati ya Taifa

11. Posho na ujira

### SEHEMU YA III

#### KATAZO LA KUTAKATISHA FEDHA HARAMU

12. Kosa la kutakatisha fedha haramu
13. Adhabu ya kutakatisha fedha haramu
14. Makosa ya mashirika/asasi

### SEHEMU YA IV

#### UDHIBITI WA UTAKATISHAJI WA FEDHA HARAMU

- 15 Watoa taarifa kuhakiki utambulisho wa mteja.
- 16 Watoa taarifa kuanzisha na kutunza kumbukumbu za mteja.
- 17 Watoa taarifa kutoa taarifa ya miamala yenye kuleta mashaka.
- 18 Watoa taarifa kuanzisha na kuendeleza taratibu za ndani za utoaji taarifa.
- 19 Taratibu za ziada za udhibiti za kutumiwa na watoa taarifa.
- 20 Tahadhari
- 21 Wajibu wa usiri.
- 22 Kuwalinda watoa taarifa.
- 23 Wajibu wa kutoa taarifa kuhusu usafirishaji wa fedha taslimu na hati huwilishi kuvuka mpaka.

### SEHEMU YA V

#### VIFUNGU VYA FEDHA

24. Vyanzo vya mapato.
25. Mwaka wa fedha.
26. Hesabu na ukaguzi.

SEHEMU YA VI  
VIFUNGU ANUWAI

- 27. Kinga.
- 28. Matumizi ya mapato yatokanayo na uhalifu.
- 29. Kanuni.

SURA YA 423

SHERIA YA KUZUIA UTAKATISHAJI WA FEDHA HARAMU

[15 Januari, 2007]

Sheria inayoweka vifungu bora vya kuzuia na kukataza utakatishaji wa fedha haramu, utoaji wa taarifa zinazohusu utakatishaji wa fedha haramu, uanzishaji wa Kitengo cha Kudhibiti Biashara Fedha Haramu na Kamati ya Taifa ya Wataalam Mbalimbali wa Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu pamoja na mambo mengineyo yanayofanana na hayo.

Sheria . Namba.423  
ya 2006

[.....]

SEHEMU YA KWANZA  
VIFUNGU VYA AWALI

- Jina fupi            1. Sheria hii itaitwa Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu ya Mwaka 2006 na itaanza kutumika tarehe ambayo Waziri atachapisha Tangazo katika gazeti la Serikali.
- Matumizi            2. Sheria hii itatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.
- Tafsiri                3. Katika Sheria hii, isipokuwa kama maudhui yatamaanisha vinginevyo:  
“Sheria” maana yake ni Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu.

Sura ya. 342 “benki” ina maana iliyotolewa katika sheria ya mabengi na Taasisi za fedha.

Sura ya .197 “benki” ina maana iliyotolewa katika Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania

“mtu anayejishughulisha na fedha” ina maana-

- (a) mtu yeyote anayefanya biashara ya kufidia majanga, dalali wa bima, muuzaji wa dhamana au wakala.
- (b) mtu afanyaye biashara inayohusisha dhahabu ghafi, kutoa, kuuza au kukomboa hundi za wasafiri, hawala za fedha na vitu vifananavyo na hivyo, au ya kukusanya, kuchukua, na kuwasilisha au kuhamisha fedha.
- (c) Mwendeshaji wa michezo ya kubahatisha,
- (d) mdhamini au msimamizi wa mfuko wa uwekezaji wa pamoja. na
- (e) Mwendeshaji biashara ya kubadili fedha.

“Mwenyekiti” ina maana ya Mwenyekiti wa Kamati ya Taifa aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 8;

“Kamishna” ina maana ya Kamishna wa Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu aliyeteuliwa katika kifungu cha 5;

“Chombo linganifu” ina maana ya wakala wa serikali wa nchi za nje mwenye majukumu yanayofanana na yale ya Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu;

Sura ya.342 “taasisi ya fedha” ina maana iliyotolewa katika Sheria ya Mabengi na Taasisi Za Kifedha

Sura ya.256 “utaifishaji” ina maana iliyotolewa katika Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu

“Serikali” ina maana ya Serikalia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Pale inapobidi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

“Waziri” ina maana ya Waziri anayehusika na mambo ya Fedha ambaye yupo Madarakani kwa sasa.

“Utakatishaji wa fedha haramu” ni kitendo cha mtu au watu kujihusisha moja Moja kwa moja au kwa njia nyingine katika kubadili, kuhamisha, kuficha , kupoteza chanzo, kutumia au kujipatia fedha au mali inayoaminika kupatikana kwa kwa njia haramu na vitendo hivyo vina lengo la kukwepa madhara ya kisheria yatokanayo na vitendo hivyo ikiwemo makosa yaliyoainishwa katika kifungu cha 12;

“Kamati ya Taifa”ina maana ya Kamati ya Taifa ya Wataalamu mbalimbali wa kudhibiti biashara ya fedha haramu iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 8;

“Mtu mwenye muelekeo wa kisiasa” ni raia wa kigeni mwenye dhamana ya kusimamia kazi za umma zinazojulikana

pamoja na wakuu wa nchi au serikali, wanasiasa waandamizi, maafisa

waandamizi wa serikali, maafisa wa mahakama au maafisa wa jeshi,

maafisa waandamizi wa wa mashirika ya umma au mawakala;  
“makosa ya uhalifu ambayo ni msingi wa utakatishaji fedha haramu” ina maana  
ya;

- (a) jambo lolote linalo husisha uingizaji na usafirishaji wa dawa haramu chini ya sheria ambayo inahusika na madawa ya kulevywa kwa wakati huu
- (b) ugaidi, ikiwa ni pamoja na kufadhili vitendo vya kigaidi;
- (c) usafirishaji haramu wa silaha;
- (d) kuhusika katika vikundi vya uhalifu wa kupangwa na ulaghai;
- (e) biashara haramu ya binadamu na usafirishaji wa wahamiaji haramu;
- (f) utumikishwaji wa kingono, ikiwa ni pamoja na utumikishwaji wa kingono wa watoto;
- (g) usafirishaji wa bidhaa haramu za wizi na bidhaa nyinginezo;
- (h) vitendo vya rushwa;
- (i) kugushi;
- (j) unyanganyi wa kutumia silaha;
- (k) wizi;
- (l) utekaji nyara, kumuweka mtu kizuizini kinyume na sheria, kuchukua mateka;
- (m) magendo;
- (n) kujipatia fedha au mali kwa vitisho;
- (o) Kugushi nyaraka;
- (p) Uharamia;
- (q) Utekaji nyara;
- (r) Kujinufaisha na taarifa za ndani na kumiliki soko;
- (s) Usafirishaji haramu wa viungo vya binadamu;
- (t) Uwindaji;
- (u) Ukwepaji wa kodi;
- (v) Uvuvi haramu;
- (w) Uchimbaji haramu wa madini;
- (x) Uhalifu wa mazingira; au
- (y) kosa lolote ambalo Waziri atalitaja kupitia Gazeti la Serikali, ikiwa limefanyika ndani au nje ya mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Sura ya 256

“mali” ina maana iliyotolewa katika sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu

“Msimamizi ” ni pamoja na Benki Kuu ya Tanzania, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Kitengo cha Usimamizi wa Bima, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha au msimamizi yeyote ambaye waziri atamtaja kupitia agizo litakalo chapishwa kupitia Gazeti la Serikali;

“mtoa taarifa” ina maana ya-

- (a) mabenki na taasisi za kifedha;
- (b) Muuzaji wa fedha;
- (c) mhasibu, wakala wa kuuzaji ardhi, muuza madini, kazi za sanaa au chuma;
- (d) msimamizi;
- (e) afisa forodha;
- (f) mawakili, maafisa wa viapo na wataalamu wengine wakujitegemea wa sheria wakati:

(i) wa kusaidia wateja katika kuandaa au kutekeleza miamala inayohusisha:

- (aa) ununuzi au uuzaji wa ardhi au mashirika ya biashara
- (bb) usimamizi wa fedha, dhamana, au mali nyinginezo zilizo katika milki ya mteja.
- (cc) ufunguzi au usimamizi wa akaunti za benki, akaunti za akiba au orodha ya fedha zilizowekwa kwa faida;
- (dd) mfumo wa ukusanyaji wa michango inayohitajika katika kuanzisha, kusimamia na kuelekeza mashirika au taasisi za kisheria
- (ee) uanzishaji, usimamizi, au uelekezaji wa Mashirika au taasisi za kisheria; na
- (ff) ununuzi au uuzaji wa taasisi za kibiashara;

(ii) kumuwakilisha mteja katika kila muamala wa fedha au ardhi;

(g) Madalali; na

(h) mtu yeyote ambaye Waziri atamueleza bayana katika tangazo litakalo chapishwa katika Gazeti la Serikali;

“ufadhili wa ugaidi” ina maana ya-

- (a) utoaji, au kusaidia upatikanaji wa fedha au huduma nyinginezo kwa gaidi, au kikundi au taasisi inayojihusisha na kitendo cha kigaidi; au
- (b) kuingia katika au kuwezesha miamala ya fedha kwa njia moja au nyingine inayohusiana na mali inayomilikiwa au kusimamiwa na au kwa niaba ya gaidi yoyote au taasisi inayomilikiwa au kusimamiwa na gaidi.

**SEHEMU YA II**  
**KITENGO CHA KUTHIBITI BIASHARA YA FEDHA HARAMU**  
**NA KAMATI YA TAIFA**

Uanzishwaji wa Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya fedha haramu 4.-(1) Kutakuwa na kitengo cha ziada cha wizara katika Wizara ya Fedha kitachojulikana kama Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu pia kitatambulika kwa kifupi kama FIU.

(2) Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu kitakuwa na kazi ya kupokea kuchanganua na kusambaza taarifa zote za miamala yenye mashaka na taarifa muhimu zinazohusiana na utakatishaji wa fedha haramu au taarifa za ufadhili wa ugaidi zilizotelewa na mtoa taarifa au vyanzo vingine ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Uteuzi wa Kamishina 5-(1) Rais atamteua mtu ambaye ana elimu ya kutosha na uzoefu katika

uchumi, masuala ya fedha, usimamizi wa fedha, sheria, makosa ya jinai ya kuichumi au eneo lolote lenye tija katika utekelezaji majukumu kulingana na sheria hii, kama Kamishina wa Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu

(2) Kamishina ndiye atakayekuwa mtendaji mkuu wa Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu.

Mamlaka na majukumu ya Kitengo 6. Kwa madhumuni ya kifungu cha 4, Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu Kitakuwa na Majukumu ya-

Cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu (a) kupokea na kuchanganua taarifa zenye mashaka zilizowasilishwa na watoa taarifa kulingana na kifungu cha 17;

(b) kupeleka taarifa yoyote kwa mawakala wanaohusika na utekelezaji wa sheria kama baada ya kupitia na kuridhika na taarifa hiyo, Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu kina sababu za kutosha kuhisi kwamba muamala unahusisha fedha haramu au kosa la uhalifu ambalo ni msingi wa utakatishaji wa fedha haramu;

(c) kupeleka kwa mawakala husika wa kusimamia sheria taarifa yoyote iliyotokana na ukaguzi uliofanyika kwa mujibu wa kipengele (d) kama taarifa hiyo inatoa au inaipa kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu sababu za msingi za kutilia shaka muamala unaohusisha mapato ya uhalifu au ufadhili wa ugaidi;

- (d) kumuelekeza mtoa taarifa kuchukua hatua zitakazofaa kufanikisha ukaguzi unaotarajiwa kufanywa na Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu;
- (e) kukusanya takwimu na kumbukumbu, kusambaza taarifa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, au kwingineko, kutoa mapendekezo kutokana na taarifa zilizopokelewa na kushauri Kamati Kuu ya Taifa pale inapobidi;
- (f) kwa kushauriana na mamlaka za usimamizi za watoa taarifa husika, kutoa miongozo kwa mabenki, taasisi za kifedha na watoa taarifa wengine kuhusu miamala yenye kuleta mashaka, utunzaji wa kumbukumbu na wajibu wa kutoa taarifa kama invyoonyeshwa katika vifungu vya 16,17,18, na 19;
- (g) kuweka mahitaji ya mafunzo na kutoa mafunzo kwa watoa taarifa, maofisa wa mahakama na maofisa wa usimamiaji wa sheria;
- (h) kushauriana na mtu yeyote anayehusika, taasisi au shirika kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa majukumu yake chini ya kifungu hiki;
- (i) kubadilishana taarifa na vitengo vya Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu vya nje ya nchi na vyombo linganifu wakala na;
- (j) kushirikiana na mamlaka husika za uwekezaji na Usajili na Utoaji wa Leseni za Biashara katika kutambua wawekezaji wa ukweli

;

Wafanyakazi wa  
kitengo cha  
kudhibiti  
Biashara  
ya fedha  
haramu

7.-(1) Watateuliwa watumishi wa Serikali au taasisi za umma kulingana idadi, aina na vigezo kama itavyohitajika ili kumsaidia kamishina katika utendaji wa kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu.

- (2) katika uteuzi wa wafanyakazi, mamlaka ya uteuzi inapaswa Kuzingatia watu wenye uzoefu katika masuala ya sheria, usimamizi wa fedha, forodha na utekelezaji wa sheria.
- (3) watumishi waliozungumziwa katika kifungu kidogo cha (1) watahikilia nafasi hizo kwa kipindi cha miaka mitano na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine.
- (4) wafanyakazi wa Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu Watatakiwa kutoa tamko la awali na kila baada ya muda flani kuhusu taarifa za mapato yao kwa namna ambayo itaagizwa katika kanuni.

Uanzishwaji na  
Muundo wa

8.-(1) kwa madhumuni ya sheria hii kutakua na Kamati ya Taifa ya Wataalam mbalimbali wa Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu.



- (2) Kamati ya Taifa itajumuisha-
  - (a) Mwakilishi mmoja wa Benki Kuu ya Tanzania ambaye ndiye atakuwa Mwenyekiti,
  - (b) Mwakilishi mmoja wa Wizara ya Fedha;
  - (c) Mwakilishi mmoja wa Wizara ya Fedha ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;
  - (d) Mwakilishi mmoja wa ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
  - (e) Mwakilishi mmoja wa ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;
  - (f) Wawakilishi wawili wa ofisi ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai, mmoja kati yao hao ni lazima atoke ofisi ya Zanzibar;
  - (g) Mwakilishi mmoja wa Wizara ya Mambo ya Nje;
  - (h) Kamishina wa Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu;
  - (i) Mwakilishi mmoja wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana;
  - (j) Mwakilishi mmoja wa Idara ya Usalama wa Taifa.
- (3) Kamati ya Taifa inaweza kumchagua mtu yeyote mwenye ujuzi maalum Au uzoefu katika upelelezi wa masuala yanayohusiana na utakatishaji wa fedha haramu.
- (4) Wajumbe wa Kamati ya Taifa iliyoanzishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) watateuliwa na waziri.
- (5) Waziri anaweza kumteua mtumishi yeyote kutoka utumishi wa umma Kuwa Katibu wa Kamati ya Taifa.
- (6) Wajumbe wa Kamati ya Taifa watahika nafasi hizo kwa muda wa miaka mitatu lakini wanaweza kuteuliwa tena kwa awamu nyingine.

- |                         |  |
|-------------------------|--|
| Kazi za Kamati ya Taifa | <p><b>9.</b> Tume ya Taifa itakuwa na kazi zifuatazo-</p> <ol style="list-style-type: none"><li>(a) kutunga , kutathmini na kuboresha ufanisi wa sera na njia za kuzuia utakatishaji wa fedha haramu;</li><li>(b) kuishauri Serikali katika utungaji, usimamizi na marekebisho ya sera zinazohusiana na kuzuia utakatishaji wa fedha haramu pamoja na kuzuia makosa ya uhalifu ambayo ni msingi wa utakatishaji wa fedha haramu.</li><li>(c) Kwa ujumla,kuishauri serikali kuhusu masuala mengine yanayohusu Utakatishaji wa fedha haramu na makosa mengine ya uhalifu ambayo Ni msingi wa utakatishaji wa fedha haramu.</li></ol> |
| Vikao vya               | <p><b>10.</b>-(1) Wajumbe wa Kamati ya Taifa watamchagua mmoja miongoni mwao Kuwa Makamu Mwenyekiti.</p>   |
| Kamati ya Taifa.        | <p>(2) Mwenyekiti atakuwa kiongozi wa mikutano yote ya Kamati ya Taifa Na asipokwepo makamu mwenyekiti atashika nafasi hiyo.</p>   |

- (3) Ikiwa mwenyekiti na makamu mwenyekiti hawapo, wajumbe waliopo wanaweza kuteua mmoja wao kuendesha kikao.
- (4) Akidi ya kikao chochote cha Kamati ya Taifa itatimia kukiwa na wajumbe Wengi.
- (5) Kamati ya Taifa itajiwekea taratibu za kuendesha vikao vyake yenyewe.

Posho na Mishahara **11.**-(1) Wajumbe wa Kamati ya Taifa watalipwa posho na marupurupu pamoja na malipo mengineyo kama itakavyoamuliwa na Waziri.

### SEHEMU YA III

#### KATAZO LA UTAKATISHAJI FEDHA HARAMU

Kosa la kutakatisha fedha haramu **12.** Mtu yeyote atakaye-

- (a) jihusisha, moja kwa moja au kwa njia nyingine katika muamala unaohusisha mali itokanayo na ya mapato ya fedha haramu akiwa anafahamu au anapaswa kufahamu au alipaswa kufahamu mali hiyo ni ya mapato yatokanayo na makosa ya uhalifu ambayo ni msingi wa utakatishaji wa fedha haramu;
- (b) badili,hamisha,safirisha, pitisha mali ikiwa anafahamu au anapaswa kufahamu au alipaswa kufahamu kuwa mali hiyo ni ya mapato yatokanayo na uhalifu ambayo ni msingi wa utakatishaji wa fedha haramu, kwa malengo la kuficha, kupoteza ukweli au chanzo halisi cha mali hiyo kuwa ni haramu au kumpa msaada mtu yeyote aliye husika katika kufanya kitendo hicho kwa lengo la kukwepa madhara ya kisheria;
- (c) ficha, funika ukweli, zuia upatikanaji wa ukweli, chanzo,mahali,Uhamishaji wa umiliki, mzunguko, au umiliki wa au haki kuhusiana na mali hiyo, akiwa anafahamu au anapaswa kufahamu au alipaswa kufahamu kuwa mali hiyo imepatikana kwa mapato yatokanayo na fedha haramu
- (d) jipatia, miliki, tumia au simamia mali, ikiwa anafahamu, au anapaswa kufahamu au alipaswa kufahamu wa kupokea mali hiyo kuwa mali hiyo imetokana na makosa ya uhalifu amabyo ni msingi wa utakatishaji wa fedha haramu; au
- (e) shiriki katika, jihusisha na, kula njama ya kutenda, jaribu kutenda, saidia au shiriki au wezesha na shauri utendwaji wa jambo lolote lililoelezwa katika aya (a) hadi (d) ya kifungu hiki atakuwa amefanya kosa la kutakatisha fedha haramu.

Adhabu za makosa ya kutakatisha

fedha haramu **13.** Mtu yeyote atayevunja kifungu cha 12 cha sheria hii, ikiwa atakuwa na hatia:  
 (a)Ikiwa ni mtu kawaida atahukumiwa kulipa faini isiyozidi shilingi milioni mia

Tano za kitanzania na isiyopungua shilingi milioni mia moja za kitanzania au kifungo kisichozidi miaka kumi au kupungua miaka mitano; au

(b) ikiwa ni shirika, shirika hilo litatakiwa kulipa faini isiyozidi shilingi za kitanzania bilioni moja na isiyopungua shilingi milioni mia tano au kuamriwa kulipa kiwango sawa na mara tatu ya thamani halisi ya mali katika soko, chochote kitakachokuwa kikubwa.

Makosa ya mashirika 14.-(1) Ikiwa kosa katika kifungu cha 12 limetendwa na taasisi au asasi ya watu, mtu yeyote ambaye, wakati kosa hilo linatendeka alikuwa-

(a) mkurugenzi, meneja, msimamizi au mbia; au

(b) alihusika katika uongozi,

anaweza kutiwa hatiani kwa kosa hilo na atawajibika kulipa faini kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 13 isipokuwa akithibitisha kuwa kosa hilo lilitendeka bila ridhaa yake au hakulifumbia macho na alifanya juhudi ya kuzuia kutendeka kwa kosa kama alivyopaswa kufanya, kwa kuzingatia majukumu yake katika nafasi hiyo na mazingira yaliyofungamana na utendaji wa kosa.

(2) Mkurugenzi, meneja, msimamizi, mbia au mtu yeyote anayehusika katika Usimamizi wa shughuli za shirika au jumuiya anaweza kutiwa hatiani kwa kosa chini ya kifungu kidogo cha (1) bila kujali kuwa shirika hilo au jumuiya hiyo haijatiwa hatiani kwa kosa hilo.

(3) mtu yeyote ambaye angeweza kutenda kosa kama angetenda kitendo chochote au angeacha kutenda kitendo chochote, ametenda kosa hilo na atakapotiwa hatiani atapewa adhabu sawa kama vile kitendo hicho kimetendeka au hakikutendeka na wakala wake au afisa akiwa katika ajira yake kama itakavyokuwa mpaka tu atakapodhibitisha kwamba kosa lilitendwa bila yeye kujua na alichukua tahadhari zote muhimu kuzuia kufanyika, au kutokufanyika kwa kitendo hicho.

#### SEHEMU YA IV

##### USIMAMIZI DHIDI YA UTAKATISHAJI WA FEDHA HARAMU

15.-(1) Mtoa taarifa anapaswa:

Watoa taarifa (a) kuchukua hatua za kutosha kujiridhisha na utambuzi na muombaji yoyote Anayetaka kuingia naye katika mahusiano ya kibiashara au kufanya muamala au miamala mfululizo, kwa kumtaka muombaji kutoa taarifa rasmi kuhakiki utambulisho wa mteja ambayo inaweza kutoa utambulisho wa muombaji

(b) kuhusiana na mtu mwenye muelekeo wa kisiasa, zaidi ya uchunguzi yakinifu kufanyika mto taarifa anapaswa;

(i) kuwa na mifumo inayofaa ya usimamizi wa vihatarishi ili kubainisha kama mteja ni mtu mwenye muelekeo wa kisiasa;

- (ii) kupata ridhaa ya viongozi waandamizi kabla ya kuanzisha mahusiano ili kuanzisha biashara na mteja huyo;
- (iii) kuchukua hatua stahiki ili kuweza kujua chanzo cha mali au chanzo cha fedha hizo; na
- (iv) kuzidisha uratibu endelevu wa uhusiano huo wa kibiashara.

(2) kumbukumbu rasmi zinazotajwa chini kifungu kidogo cha (1)

Ni pamoja na:

- (a) cheti cha kuzaliwa au kiapo cha kuzaliwa
- (b) hati ya kusafiria au njia nyingine za rasmi utambulisho
- (c) ikiwa ni shirika, nakala ya katiba ya shirika na hati ya usajili pamoja na taarifa za mwaka za hivi karibuni zilizothibitishwa na Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Usajili na Utoaji wa Leseni za Biashara; na
- (d) nyaraka nyingine zozote kama itakavyoagizwa na Waziri katika kanuni.

(3) pale muombaji atakapoiomba benki, taasisi ya fedha au mtoa taarifa

Mwingine yeyote kuingia katika:

- (a) mahusiano ya kibiashara endelevu
- (b) ikiwa hakuna mahusiano ya aina hiyo, muamala wowote, benki, taasisi ya kifedha au mtoa taarifa yeyote anapaswa kuchukua hatua za msingi kuthibitisha kama mtu huyo ana muwakilisha mtu mwingine.

(4) ikiwa itaonekana kwa mtoa taarifa kuwa muombaji ameomba kuingia katika muamala wowote, kama katika mahusiano ya kibiashara endelevu au la, anaomba kwa niaba ya mtu mwingine, mtoa taarifa anapaswa kuchukua hatua za msingi kuthibitisha utambulisho halisi wa mtu yoyote ambaye muombaji anaomba kwa niaba yake au ambaye muombaji anaomba kwa faida yake katika muamala uliopendekezwa, ikiwa kama ni mdhamini, mteuliwa, wakala au vinginevyo.

(5) Katika kuamua nini kinajumuisha hatua za msingi kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1), (2), au (4) mazingira ya jambo husika lazima yazingatiwe na hususan;

- (a) ikiwa kama muombaji ni mtu wa binafsi au ni shirika ambalo limesajiliwa katika nchi ambayo kuna sheria inayozuia matumizi ya mifumo wa fedha kwa lengo la kutakatisha fedha haramu au kufadhili ugaidi;na
- (b) desturi na taratibu zitakazokuwepo muda hadi muda katika nyanja husika ya biashara.

(6) Hakuna kitu katika kifungu hiki kitakachohitaji kutoa ushahidi

Wowote wa utambulisho pale ambapo-

(a) muombaji mwenyewe ndiye mtoa taarifa pale ambapo sheria hii inatumika

(b) kuna muamala au miamala mfululizo inayofanyika katika mahusiano ya biashara, kwa sababu hiyo muombaji ameshatoa ushahidi wa kuridhisha wa utambulisho wake.

Mtoa taarifa kuanzisha na kutunza kumbukumbu za mteja

16.-(1) Kila mtoa taarifa anapaswa kuanzisha na kutunza-

a) kumbukumbu za miamala yote za kiwango cha sarafu au kiwango kinacholingana na hicho katika sarafu za kigeni kama itakavyobainishwa na waziri katika agizo lililochapishwa kupitia Gazeti la Serikali, linaloelezea mambo yakufanywa na mtoa taarifa kwa mujibu wa matakwa ya kifungu kidogo cha (3); na

(b) Ambapo ushahidi wa utambulisho wa mtu utapatikana kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha (15), kumbukumbu inayoonyesha aina ya ushahidi uliopatikana, na ambayo ndani yake ina nakala ya ushahidi au taarifa ambayo inaweza kupelekea upatikanaji wa nakala hiyo.

(2) kumbukumbu zinazohitajika chini ya aya (a) ya kifungu kidogo cha (1) Zitajumuisha taarifa za kutosha kumtambulisha mtu:-

(a) jina, anuani na kazi au pale itapofaa biashara au kazi kuu ya kila mtu:-

(i) anayefanya muamala;

(ii) ikiwa imejulikana, biashara inafanyika kwa niaba ya nani, na njia ambazo zimetumiwa na mtoa taarifa katika kuhakiki utambuzi wa mtu huyo.

(b) Asili na tarehe ya muamala;

(c) aina ya sarafu na kiwango kilichohusika;

(d) aina na namba ya utambulisho wa akaunti yoyote na mtoa taarifa aliyehusika katika muamala;

(e) iwapo muamala huo unahusisha hati huwilishi na si sarafu, jina la mtu anayetoa hati, jina la taasisi ambayo hati hiyo imetolewa, jina la mtu anayelipwa kama lipo, kiasi cha fedha na tarehe ya hati, namba ya hati kama ipo, na maelezo yoyote ya uidhinishaji yaliyopo katika hati; na

(f) jina na anuani ya mtoa taarifa, na afisa, mwajiriwa, wakala wa mtoa taarifa ambaye ndiye aliyehandaa kumbukumbu.

(3) mtoa taarifa anapaswa kuweka kumbukumbu zinazotakiwa chini ya kifungu kidogo cha (1) kwa kipindi ambacho Waziri ataelekeza katika Kanuni.

(4) pale ambapo mtoa taarifa anatakiwa na kifungu chochote cha sheria kutoa nyaraka ya aina yoyote iliyotajwa katika kifungu cha 18 kabla ya kipindi kilicho elekezwa na Waziri, atatakiwa kubakiza nakala ya nyaraka hiyo na anapaswa pia kutunza daftari la kumbukumbu la nyaraka zote zilizotolewa zikiwa na taarifa zote kama itakavyoelekezwa katika kanuni zitakazotungwa.

Watoa taarifa

17.-(1) Ikiwa mtoa taarifa atakuwa na mashaka au anayo sababu ya kuwa Na mashaka kwamba, fedha au mali ni mapato yatokanayo na uhalifu, Kutoa au yana husiana au kuunganishwa au yatatumika katika kutenda au Kuendeleza makosa ya uhalifu ambayo ni msingi wa utakatishaji wa fedha haramu au ana

taarifa ya Miamala  
yenye kuleta

Mashaka

uelewa wa jambo au shughuli ambayo inaweza kuwa ishara ya utakatishaji fedha au makosa ya uhalifu ambayo ni msingi wa utakatishaji wa fedha haramu anapaswa, ndani ya masaa ishirini na nne baada ya kutilia shaka, na haraka iwezekanavyo, kabla muamala haujafanyika;

- (a) kuchukua hatua za msingi kuhakikisha dhumuni la muamala au muamala uliopendekezwa, chanzo, kikomo cha fedha au mali inayohusika, na utambuzi na anuani ya kila mnufaika wa mwisho; na
  - (b) kuandaa taarifa ya muamala au muamala uliopendekezwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2), na kuwasilisha taarifa hiyo kwenye Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu kwa njia yeyote salama kama itakavyoelekezwa na Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu.
- (2) taarifa inayotakiwa katika kifungu kidogo cha (1) ni lazima iwe na Maelezo kama itakavyoelekezwa katika kanuni zitakazotungwa.
- (3) Mtoa taarifa ambaye ametoa taarifa ya muamala wenye mashaka au muamala uliopendekezwa wenye mashaka kwa mujibu wa sehemu hii anapaswa, ikiwa ameombwa kufanya hivyo na Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu au taasisi ya utekelezaji wa sheria inayo chunguza muamala wenye mashaka, kutoa taarifa zaidi kuhusiana na muamala huo.
- (4) mtu yoyote atakayekiuka kifungu kidogo cha (1) cha sheria, akikutwa na Hatia;
- (a) ikiwa ni mtu binafsi, atalipa faini isiyozidi shilingi milioni tano au kifungu kwa kipindi kisicho zidi miaka mitano;
  - (b) ikiwa ni shirika, litatakiwa kulipa faini isiyozidi shilingi milioni kumi au kiwango ambacho ni sawa na mara tatu ya thamani ya mali husika katika soko, chochote kitakachozidi kingine .

watoa  
taarifa kuanzisha  
na kuendeleza  
taratibu za  
ndani  
za utoaji taarifa

**18. Mtoa taarifa anapaswa kuanzisha na kuendeleza mfumo wa kutoa taarifa wa ndani;**

- (a) kwa kuteua mtu ambaye waajiriwa wake watampelekea taarifa zozote zinazohusu muamala wenye kutia mashaka ambao waajiriwa wameubaini wakiwa katika ajira kwamba mtu anahusika katika kutakatisha fedha au kitendo kinachopelekea makosa ya uhalifu ambayo ni msingi wa fedha haramu

- (b)kwa kumuwezesha mtu aliyeteuliwa kupata taarifa ambazo zinaweza kuwa muhimu katika kuamua kama kuna msingi wa kuridhisha wa kutolewa taarifa kulingana na kifungu cha 17 (1); au
- (c) kwa kumtaka mtu aliyeteuliwa kutoa taarifa kulingana na kifungu cha 17, katika tukio ambalo ataamua kuna sababu za kutosha.

Taratibu za  
ziada  
za udhibiti  
za kutumiwa

**19.-(1)** Zaidi ya masharti yaliyotajwa chini ya kifungu cha 18 mtoa taarifa anapaswa;

(a) kufata taratibu zinazofaa kwa lengo la kuwafahamisha waajiriwa sheria za ndani ya nchi zinazohusika na utakatishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi,na mienendo na sera zilizoanzishwa na kuendelezwa na mtoa taarifa kuhusiana na sheria hii.

na

watu

(b)Kuwapa waajiriwa mafunzo yanayofaa katika kutambua na kushughulikia miamala inayohusiana na utakatishaji wa fedha haramu au ufadhili wa ugaidi;

(2) Mtu yeyote hapaswi kufungua au kuendesha akaunti katika benki, au taasisi ya fedha au mtoa taarifa mwingine yeyote kwa kutumia jina la uongo, lililofichwa au bila jina.

(3) Benki, taasisi ya fedha au mtoa taarifa yoyote atakaye fanya kosa chini Ya sehemu hii,ambayo adhabu haijatajwa,akikutwa na hatia;

(a) ikiwa ni mtu binafsi, atatakiwa kulipa faini isiyozidi milioni tano au kifungu cha miezi kumi na mbili; na

(b) ikiwa ni shirika, litawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi milioni kumi.

(4) Katika kuamua kama mtu amefuata masharti ya sheria katika kifungu Kidogo cha (1), mahakama itapaswa kuzingatia mazingira yote ya kesi, ikiwa ni pamoja na desturi na taratibu ambazo toka muda hadi muda huwa zinatumiwa katika biashara, weledi au ajira, pia inaweza kufikiria miongozo yoyote husika iliyoasiliwa au kudhibitishwa na mamlaka ya umma au shirika lingine linalosimamia, dhibiti, au mwakilishi wa biashara, weledi, au ajira inayofanywa na huyo mtu.

Utoajii wa  
siri za  
ndani

**20.-(1)** Mtu yeyote hatakiwi kutoa taarifa au tahadhari kwa mtu yeyote anayehusika katika muamala,au kwa mtu wa tatu asiyeruhusiwa,wakati wa kuanzisha au kwenye mahusiano ya uteja au wakati wa kufanya miamala ya mara chache-

(a) kwamba, taarifa ya muamala wenye mashaka chini ya kifungu cha 17 inaweza kuandaliwa, au inaandaliwa au imetumwa kwenye Kitengo cha

Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu; au

(b) Taarifa nyingine yeyote au jambo, isipokuwa hadi itakapohitajika na sheria Hii.

(2) mtu yeyote atakayekiuka kifungu kidogo cha sheria cha (1) akikutwa na Hatia:

(a) ikiwa ni mtu binafsi, atatakiwa kulipa faini isiyozidi shilingi milioni mia tano na isiyopungua shilingi milioni mia moja au kifungu kwa kipindi kisichozidi miaka kumi na kisichopungua miaka mitano;

(b) Ikiwa ni shirika, litatikiwa kulipa faini isiyozidi shilingi bilioni moja na isiyopungua shilingi milioni mia tano au mara tatu ya thamani ya mali katika soko,chochote kitakachozidi kingine.

(3) katika mwenendo wa kosa chini ya kifungu kidogo cha (1), itakuwa ni utetezi kuthibitisha kwamba, mtu hakufahamu au ana sababu za msingi za kudhani kwamba, utoaji taarifa hiyo ungeweza kuathiri uchunguzi wowote wa utakatishaji fedha haramu na makosa ya uhalifu ambayo ni msingi wa fedha haramu

Kuondoshwa  
wajibu wa usiri

**21.**-(1) Vifungu vya sehemu hii vitafanya kazi, bila kujali wajibu wa usiri au mazuio mengine, katika utoaji wa taarifa uliowekwa na sheria yeyote au vinginevyo.

Ulinzi wa mtoa taarifa na shahidi

**22.**-(1) Bila kujali sheria yoyote, hakuna hatua ya kisheria, shauri au mwenendo Wowote utakaochukuliwa dhidi ya mtoa taarifa yoyote au mkurugenzi yoyote, au afisa, mwajiriwa au mwakilishi wa mtoa taarifa katika misingi ya kukiuka maadili ya kibenki au weledi wa usiri au kwa sababu ya hasara yoyote itokanayo na uchunguzi,uendeshaji wa mashitaka au hatua nyingine za kisheria zilizochukuliwa dhidi ya mtu yoyote, au kufuatia taarifa au habari iliyopelekwa kwa nia njema chini ya sehemu hii, ikiwa mashaka hayo yalithibitika au hayakuthibitika.

(2) katika mwenendo wa shauri lolote la jinai lililoletwa chini ya sheria hii, baada ya ombi la mwanasheria mkuu mahakama inaweza kuamuru:

(a) ushahidi kutolewa kwa kupitia teknolojia ya mawasiliano kama vile njia ya video

(b) kutokutaja au kuweka mipaka katika utambuzi na mahali alipo shahidi ili kuzingatia usalama wa mtoa habari huyo au shahidi; au

(c) Amri ya ulinzi wa aina yoyote ambao mahakama utaona sawa, baada ya ombi la Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(3) Maelezo ya kifungu kidogo cha sheria cha (1) katika kifungu hiki



Yatatumika kwa sawia kwa waathirika ikiwa ni mashahidi

Wajibu wa kutoa taarifa kuhusu Usafirishaji wa fedha au hati huwilishi kuvuka mpaka

**23.**-(1) Mtu yeyote, atakayeingia au kutoka eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa anasafirisha au anakaribia kusafirisha, ameshasafirisha fedha au hati huwilishi katika kiwango sawa au kilichozidi kiwango kilicho agizwa na Waziri katika kanuni, itakuwa wajibu wa mamlaka za forodha ambazo zitawasilisha taarifa hizo kwenye Kitengo cha Kuthibiti Biashara ya fedha haramu.

(2) Mamlaka za forodha zitakuwa na mamlaka ya kutwaa kiwango chote cha fedha au hati huwilishi ambazo taarifa zake hazikuwasilishwa.

(3) Ikiwa mtu yeyote atashindwa kutekeleza wajibu wa kutoa taarifa ulitolewa na Kifungu kidogo cha (1), mamlaka yenye uwezo inaweza kutoa adhabu yoyote ya kiutawala dhidi ya mtu huyo.

#### SEHEMU YA V VIFUNGU VYA FEDHA

Vyanzo vya mapato

**24.** Mapato ya Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu ni pamoja na-

(a) kiasi cha fedha ambacho iliyoidhinishwa na bunge; na

(c) misaada na michango iliyopokelewa kwa kufuata sheria na Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu.

Mwaka wa fedha

**25.** Mwaka wa fedha wa Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu Utakuwa kipindi cha miezi kumi na mbili ya kalenda kuanzia siku ya kwanza ya mwezi julai kila mwaka.

Hesabu na ukaguzi

**26.**-(1) Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu kinatakiwa kutunza Hesabu na kumbukumbu za miamala na shughuli zake na kuhakikisha kuwa fedha zote zilizopokelewa zinawekwa katika hesabu sahihi na na malipo yote kutoka katika fedha zake yanafanywa na kuidhinishwa kwa usahihi na madaraka juu ya kutosha juu ya mali zake yanadumishwa.

(2) Kamishina anatakiwa haraka iwezekanavyo lakini sio zaidi ya siku tisini baada ya siku ya thelathini ya mwezi Juni ya kila mwaka, kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu na kumbukumbu za fedha za Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu, ambaye atakagua kuandaa taarifa ya hesabu

SEHEMU YA VI  
VIFUNGU ANUWAI

Kinga

27. Hakuna hatua ya kisheria itakayochukuliwa dhidi ya Kitengo cha Kuthibiti Biashara ya Fedha Haramu, Kamishina, Wajumbe wa Kamati ya Taifa au wafanyakazi wa Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu kwa kufanyika au kutokufanyika kwa kitendo kwa nia njema katika kutekeleza kazi za Kitengo Cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu, chini ya sheria hii na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.

28. Taratibu zote zinazohusiana na kumkamata mtu, mamlaka ya ukusanyaji wa taarifa, daawa, uamuzi, utaifishaji, adhabu ya kunyanganywa mali, adhabu ya fedha na amri ya zuio na udhibiti wa mali inayopaswa kutaifishwa, utakuwa kwa mujibu wa vifungu vya Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.

Kanuni

29.-(1) Waziri anaweza kutengeneza kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa madhumuni na vifungu vya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri ujumla wa kifungu kidogo cha (1), Waziri anaweza Kutengeneza kanuni kugiza:

(a) mambo yanayohitaji au kuruhusiwa kuagizwa na sheria hii; .

(b) mambo ambayo ni muhimu au yanayofaa kuagizwa kwaajili ya utekelezaji wa utimizaji sheria hii.